**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

**SHULE YA SEKONDARI RUNGWE**

**MAWASILIANO: - (i) MKUU WA SHULE - 0789 - 033 331 / 0739-033 331**
**(ii) MAKAMU MKUU WA SHULE - 0754 – 097 776 / 0719-049 408**

**Kumb.Na.RSS/F.5SEL. /221/…….**

Ndugu………………………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUNGWE MWAKA …………..**

Ninafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule ya Sekondari Rungwe mwaka **...................** katika combination ya ……………….

Shule ya Sekondari Rungwe ipo umbali wa Km.16, Magharibi mwa Mji mkuu wa Wilaya ya Rungwe.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe .................. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe **......................** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **.....................** Aidha unatakiwa kufuata maelekezo ya wizara ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa **(OR-TAMISEMI)** kuhusu tarehe halisi ya kuanza kuripoti na tarehe ya mwisho ya kuripoti kama itakuwa tofauti na tarehe zilizotajwa hapo juu.

**HALI YA HEWA NA JINSI YA KUFIKA SHULENI.**

Shule ya Sekondari Rungwe iko Mkoani Mbeya,Wilaya ya Rungwe, shule ipo umbali wa kilometa 45 kutoka Mbeya Mjini. Toka Tukuyu kilometa 16. Aidha Shule iko chini ya Mlima Rungwe wenye urefu wa Meta 2981 A.S.L.

Hali ya hewa ni ya baridi na mvua kwa kipindi kirefu. Hali hii ni nzuri sana kwa afya ya mwanafunzi na ni mazingira mazuri kwa kujifunzia.

Ili ufike shuleni vipo vituo vya kushukia katika barabara kuu itokayo Mbeya Mjini kuelekea Kyela, telemka kwenye mji mdogo wa **KIWIRA** utapata usafiri wa **TAX** Tshs. **20,000/=**

Pia ukishuka kituo cha **KIKOTA** ni jirani zaidi, utapata usafiri wa **BODABODA** kwa **Tshs. 3,000/=.**

**MAAGIZO MBALIMBALI.**

1. **SARE YA SHULE**:

(a) Suruali 2, kitambaa cha tetron. Rangi ya dark blue suruali (moja) na rangi ya kijivu suruali (moja). Mzazi umshonee mwanao suruali hizo pamoja na tai zake kwa kuzingatia vipimo viliyoainishwa katika kipengele (**h**) hapa chini. Aidha, kwa mzazi atakayeoona inafaa, anaweza kuzipata Suruali hizo pamoja na tai zake hapahapa shuleni kwa bei ya Tshs. 25,000/= kwa kila moja. Hata hivyo rangi za suruali hizo zimeambatanishwa kwenye barua hii ya kujiunga ukurasa wa 9. Aje na Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi usiokuwa na mapambo.

(b) Mashati mawili meupe mikono mirefu na marefu kurahisisha

kuchomekea yasiyo na mapambo au nembo yoyote.

(c) Viatu vyeusi jozi mbili vyenye kisigino kifupi vyenye kamba na visivyo chongoka sana mbele.
(d) Soksi jozi mbili rangi nyeusi.
(e) Kila mwanafunzi aje na Sweta moja rangi ya **Bluu 'V'.** Aidha kwa mzazi/mlezi atakayeoona inafaa anaweza kupata sweta hilo hapa shuleni kwa **Tshs. 15,000/=**
(f) T.shirt mbili za shule rangi ya kijani zenye nembo ya shule kwa mwanafunzi anayetaka kununua shuleni zinapatikana hapa shuleni kwa Tsh. **15,000/=** kwa kila moja.
(g) Track suit ya rangi ya blue yenye mistari miuepe.
(h) Shamba dress (suruali nyeusi mbili (Tetron ) shona nyumbani.

**N.B:Vaa suruali nyeusi iwe kitambaa cha tetron yenye Malinda mawili mbele na turnup. Suruali iwe na upana wa 17cm na shati jeupe unapokuja kuripoti. Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni.**

**2. MATIBABU YA MWANAFUNZI**

a. Kila mzazi/mlezi analazimika kumkatia mwanae **BIMA YA AFYA (NHIF) na aje nayo shuleni kwa ajili ya matibabu ya mwanfunzi husika.**

b. Endapo mzazi/mlezi atashindwa kumkatia **BIMA YA AFYA** mwanae, itamlazimu ampatie mwanae fedha sh. **50,400/=** (kwa mwaka) ili akifika shuleni aweze kutengenezewa BIMA hiyo na mamlaka husika kwa ajili ya afya yake awapo shuleni.

**3. VIFAA VYA DARASANI**

- Kalamu za wino, risasi, rula, mkebe (mathematical set) daftari kubwa zisizopungua 12. (zinauzwa kwenye duka la shule) - QUIRE 3
- Bunda mbili **(2)** za karatasi kwa muhula mmoja, (zinauzwa kwenye duka la shule).
- Wanafunzi wa mchepuo wa sayansi, **PCB, PCM, PMCs & CBG, pia** mchepuo wa **EGM na HGE** waje na scientific calculator **fx991** (pia zinapatikana kwenye duka la shule kwa bei ya **Tsh.35,000/=** kwa wanaosoma **ADV. MATH** na **Tsh. 30,000/=** kwa wanaosoma **BAM)**.
- Dissecting kit kwa wanao soma somo la Biolojia.
- Kila mwanafunzi aje na vitabu kulingana na mchepuo wake (shule ina upungufu wa vitabu).
- Kila mwanafunzi wa mchepuo wa sayansi atatakiwa aje na koti jeupe la maabara.

**4. VIFAA VYA BWENINI**

- Aje na Shuka mbili rangi ya kijani, shuka moja rangi ya pink, Blanket moja, mto na foronya zake, kanda mbili jozi moja, sahani, bakuli, kikombe, kijiko kwa ajili ya chakula.
- Aje na Chandarua rangi ya bluu moja
- Toiletpaper bunda 3 kwa mzazi atakaeona ifaa anaweza kuzipata kwenye duka la shule kwa Tsh.3000/=
- Aje na Godoro la futi **$2^1/_2$ x 6.** Aidha, kwa mzazi/mlezi atakayeona inafaa anaweza kupata Godoro hilo kwenye duka la shule kwa **Tshs. 30,000** au **Tsh. 40,000/=**

**5. NGUO ZA MICHEZO**

- Jezi rangi ya bluu.
- Raba za michezo. (TRAINING SHOES).

**6. VIFAA VYA USAFI NA UZALISHAJI MALI**

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| VIFAA | - Jembe na mpini (mpini unapatikana a shuleni kwa Tshs.200)<br>- Ndoo lt.10 Mbili<br>- Ruber squiser moja | PANGA | SLASHER | HARD BROOM | HARD BROOM | SOFT BROOM |
| WAHUSIKA | WOTE | EGM | PCM | PCB | CBG | HGE, HGK, HKL, HGL (i.e. ALL ARTS) |

**NB**. Kwa wanafunzi wa **PMCs** waje na shoka lenye mpini wa chuma pamoja panga tu.

7. **MICHANGO YA SHULE.**

i. Mchango wa uendeshaji wa shule 65,000/=
ii. Tahadhari 5000/=
iii. Nembo 5000/=
iv. Kitambulisho 5000/=

**JUMLA 80,000/=**

- Lipa michango kupitia Akaunti ya shule **NMB, A/C no. 61401000007**, **A/C name HEADMASTER RUNGWE HIGH SCHOOL.**
- Mwanafunzi aje na **BANK PAYSLIP** yenye kuonesha mchanganuo wa malipo hayo. Mwanafunzi ambaye hatakuja na Bank pay in slip ya malipo hatapokelewa wala kuandikishwa.
- Michango yote tajwa hapo juu katika kipengele namba 7 utatakiwa kuweka katika akaunti hiyo hapo juu na sio vinginevyo na kuwasilisha bank payslip katika ofisi Ya Mhasibu wa shule na **hakuna malipo ya pesa taslimu.**

8. **FEDHA YA MATUMIZI BINAFSI NA NAULI YA KURUDIA NYUMBANI WAKATI WA LIKIZO**

- Ni wajibu wa kila mzazi/mlezi kuhakikisha kwamba anampatia mtoto wake fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi binafsi,dharula pamoja na nauli ya kurudi nyumbani wakati wa likizo.
- Shule haina uwezo wa kuwawekea fedha shuleni au kuwakopesha wanafunzi ambao hawatatumiwa nauli na wazazi /walezi wao wakati wa likizo**.**

9. **VITABU VYA MASOMO**:

- Shule inakabiliwa na upungufu wa vitabu vya masomo, hivyo kila mzazi/mlezi amnunulie mwanae baadhi ya vitabu muhimu kulingana na mchepuo wake.
- NB: Vitabu vyote ni vile vya kidato cha tano na sita tu vinavyouzwa kwenye maduka ya vitabu.

10. **MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA KUJA SHULENI**

- Nenda kapime afya yako kwa daktari wa hospitali ya serikali, tumia fomu iliyoambatanishwa, na uje nayo ikiwa imesainiwa na daktari.
- Soma na kuzielewa sheria na kanuni za shule ambazo zimeambatanishwa, wewe pamoja na mzazi/mlezi wako muweke sahihi kuonyesha mnakubaliana nazo.

**NB: NI MARUFUKU MWANAFUNZI KUJA NA SIMU AU LAINI YA SIMU AU KIASHIRIA CHOCHOTE CHA KUMILIKI SIMU SHULENI VINGINEVYO HATAPOKELEWA.**

……..……………………

**A. A. CHOTA**
**(MKUU WA SHULE)**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha shule ni jumuiya na inapaswa iwe na taratibu ambazo zitaiongoza jumuiya hiyo ili kufikia malengo yake kwenye ufanisi zaidi. Lengo la elimu ni kufuta ujinga na pia kuwaandaa vijana wetu kulitumikia Taifa katika sekta mbalimbali. Wajibu wa shule ni kuandaa raia wema wa baadae. Shule haitazamii kuandaa raia wavunja sheria (wahuni, wezi, majambazi n.k.). Hivyo kila mwanafunzi wa shule hii analazimika kufuata na kutenda kama sheria na kanuni zinavyooneshwa hapa chini. Ni vizuri kila mzazi/mlezi akae na mwanae na kuzisoma na kuzielewa kabla ya kuja shuleni. Baada ya kuzisoma weka sahihi yako na sahihi ya mwanafunzi. Mwanafunzi ambaye atakuja na fomu ambayo haijasainiwa na mzazi/mlezi hatapokelewa.

### A. HESHIMA:

i. Mwanafunzi atasimama na kusalimia mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri anapopita, anapoingia darasani na penginepo.
ii. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia lugha chafu wakati wowote kati yao wenyewe, kwa mwalimu na watu wengine.
iii. Mwanafunzi ni lazima awaheshimu wafanyakazi wote waliopo shuleni kwani ni walezi wake.
iv. Kila mwanafunzi ni lazima athamini na kuheshimu kazi za aina zote
v. Kila mwanafunzi ni lazima ashirikiane na wenzake katika kazi zote
vi. Ni marufuku kwa mwanafunzi kufanya yafuatayo:
   a) Kuvuta sigara au bangi na kutumia madawa ya kulevya.
   b) Kufuga kucha, ndevu na nywele ndefu.
   c) Kuvaa mavazi yasiyo ya heshima
   d) Kugombana au kupigana
   e) Kunywa pombe
vii. Mwanafunzi ataitikia mara moja anapoitwa na walimu na kukimbia mwalimu aliko.
viii. Mwanafunzi ataheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, nembo ya Taifa, wimbo wa Taifa na fedha ya taifa.
ix. Kila mwanafunzi lazima aheshimu ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula, ofisi za shule, mali yake, wenzake na mali ya umma.
x. Mwanafunzi atanyoosha mkono na kusimama wakati wa kuuliza maswali na kujibu.
xi. Kila mwanafunzi anatakiwa kukaa kimya akiwa darasani na kuomba ruhusa ya kutoka nje kwa mwalimu au kiongozi wa darasa
xii. Mwanafunzi ni lazima aheshimu viongozi wa serikali ya wanafunzi.
xiii. Mwanafunzi ni lazima awaheshimu viongozi wa serikali na watu wote.

### B. MAHUDHURIO:

i. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi kwa muda wote wa masomo ndani ya darasa.
ii. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie kazi za mikono na michezo
iii. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie shule kwa muda wote uliopangwa
iv. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie mikusanyiko yote ya shule ambapo hutolewa matangazo mbalimbali na pia kuitishwa majina (rollcall)
v. Kila mwanafunzi lazima ahudhurie mikutano ya shule kama baraza la shule, ukaguzi wa usafi kupandisha bendera ya taifa na mikutano mingine.

**C. MAANDALIO YA JIONI.**

i. Kila mwanafunzi atalazimika kufanya maandalio ya jioni katika darasa lake
ii. Walimu watatoa kazi na watahakikisha kuwa zimefanywa.

D. **KUWAHI:**

i. Kila mwanafunzi ni lazima azoee na kuthamini muda.
ii. Kila mwanafunzi ni lazima awahi mahali anapohitajika kama ratiba inavyomtaka, wanaochelewa wataadhibiwa.
iii, Mwito wa dharura ukitokea mwanafunzi ni lazima akimbilie huo mwito.
iv Kengere itagongwa ili kukujulisha muda wa kufanya shughuli mbalimbali.
v. Mwanafunzi lazima ufike shuleni kwa tarehe zilizopangwa.

E. **SARE ZA SHULE**

1. Kila mwanafunzi anatakiwa kuvaa sare kwa matukio wakati ufuatao.
   (a) Ukiwa masomoni, darasani.
   (b) Unapotoka nje ya shule
   (c) Unapo hudhuria baraza la shule
   (d) Unapo kwenda hospitali kutibiwa
   (e) Unapo kwenda kwenye maandamano
   (f) Unapo kwenda nyumbani na kurudi shuleni.
2. Kila mwanafunzi lazima awe na vazi la kufanyia kazi za mikono.
3. Kila mwanafunzi lazima awe na nguo za michezo.
4. Kofia haziruhusiwi kuvaliwa katika eneo la shule, isipokuwa kofia maalum kwa Waislamu wanapokwenda kuswali.

**F. MIPAKA YA SHULE**

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nje ya mipaka ya shule wakati wote anapokuwa shuleni, mpaka awe na kibali maalum
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi kutembelea sehemuzi fuatazo isipokuwa kwa kibali maalum.
   (a) Nyumba za walimu na staffroom
   (b) Maabara
   (c) Jikoni.
   (d) Nyumba za wafanyakazi (wasio walimu)
3. Ni mwiko kwa mwanafunzi kutembelea, kuonekana kuzoea sehemu zifuatazo:
   (a) Vilabu vya pombe
   (b) Nyumba za starehe
   (c) Nyumba za kufikia wageni.
4. Mwanafunzi haruhusiwi kulala nje ya shule isipokuwa kwa kibali cha mkuu wa Shule.

**G. USAFI:**

Usafi ni sehemu ya maisha yako na iwe ni tabia yako kuwa msafi na kushiriki kikamilifu katika kuyaweka safi mazingira ya shule.

**H. BWALO LA CHAKULA**

i. Bwalo liwe safi daima na liheshimiwe
ii. chakula kiliwe ndani ya ukumbi
iii. usiingie jikoni bila kibali cha mwalimu au kiongozi anayehusika na bwalo

iv. uwe muungwana unapokula chakula, hakuna sababu ya kuzungumza na kupiga kelele wakati wa mlo.
v. Hairuhusiwi kuingia na viatu vya wazi na ndala ndani ya Bwalo la chakula na jiko la shule.

## I. MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa /utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu ,walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
vi. Kunyoa nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni.
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
ix. Uvutaji wa sigara.
x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xii. Kusababisha mimba.
xiii. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi au kifaa kinachoashiria matumizi ya simu (chaja, earphones, line n.k) awapo katika muhula wa masomo.
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
xvii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi.

**Mwanafunzi lazima aje na picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA YA MKUU WA SHULE AU MAKAMU MKUU WA SHULE ZILIZOPO KWENYE BARUA HII YA KUJIUNGA HAPO JUU.**

**...............................**

**A. A. CHOTA**

(MKUU WA SHULE)

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI NA ANUANI**

Jina la mzazi/mlezi…………………………………………………………………...
Anuani ya nyumbani……………………………………………………………………
(physical address)
Namba ya simu ya nyumbani/mkononi …………………………………………………

**SAHIHI ……………………………………………...TAREHE…………………………...**

**SAHIHI YA MWANAFUNZI**

Nimezisoma na kuzielewa sheria na kanuni za shule na kwamba nitakuwa tayari kuzifuata.

Jina………………………………………sahihi……………………tarehe…………………….

**SAHIHI YA MKUU WA SHULE**

**JINA…………………………….…….SAHIHI……………..…TAREHE …………….**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRIME MINISTER'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.**

**RUNGWE HIGH SCHOOL**
P.O. BOX 28
**TUKUY U.**

**DATE ………….………**

To The Medical Officer
Government Hospital
**………………………………**
**………………………………**
**……………………………..**

Please examine… .....................................................as to his fitness for pursuing further education at this school.

1) Hemoglobin ………………………………………………………………………………
2) P.V.Blooding………………………………………………………………
3) (a)Blooding ……………………………………………………………
   (b) Hearing ……………………………………………………………
4) Blood pressure……………………………………………………………
5) Stool for routine examination ……………………………………………
6) Urine for sugar …………………………………………………………
7) Skindiseases………………………………………………………………
8) Leprosy ……………………………………………………………………
9) Pulmonarytuberculosis……………………………………………………
10) Asthma ……………………………………………………………………
11) Epilepsy …………………………………………………………………
12) Deformity ………………………………………………………………...
13) Mental problem …………………………………………………………...
14) Comments…………………………………………………………………
    ………………………………………………………………………..
    ………………………………………………………………………..
    ……………………………………………………………………….

**……………………………………………………..**

**DESIGNATION**

## VIAMBATANISHO VYA RANGI YA SURUALI

**RANGIYA DARK BLUE**



**RANGI YA KIJIVU**

